MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 5 TOLEO 18

DISEMBA 16, 2008

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!


MAKALA MAALUM

JINSI ATCL ILIVYOTAFUNWA!

MATTAKA NA NYANG'ANYI

KUPELEKWA KISUTU?





Na. Fred Katunzi

Mojawapo ya masimulizi ya kusikitisha ni jinsi shirika la ndege la Tanzania (ATCL) limevurugwa, kuharibiwa na kubomolewa na wale waliopewa dhamana ya kulijenga. Kwa muda wa karibu mwaka mzima tumekuwa tukiandika kwa kina juu ya ubovu na tabia ya "kujichukulia chako mapema" katika shirika hili ambapo uongozi wa David Mattaka – kushoto (Mkurugenzi Mkuu na timu yake) na Balozi Mustaffa Nyang'anyi—kulia (Mwenyekiti wa Bodi na timu yake) wameonesha uzembe, kutokujali, na udhaifu mkubwa wa kiuongozi na utendaji.



Mahujaji

Tulianza kufuatilia suala la ATCL mwaka jana (2007) baada ya kile ambacho kilijulikana kama "Sakata la Mahujaji" ambapo mamia ya mahujaji wa Tanzania waliokuwa wanaenda kwenye Ibada ya Hijja walijikuta wakikwama kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Julius K. Nyerere kwa siku kadhaa baada ya kukosa ndege ya kuwapeleka Saudi Arabia licha ya kuwa wamelipa gharama zote na kuhakikishiwa safari yao na mawakala wao na kampuni ATCL.

Baadaye tulikuja kugundua kuwa kukwama kwa mahujaji wale kulisababishwa na woga wa Bw. Mattaka ambaye (inaendelea Uk 2.-3)



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- Kinatoka kila Jumanne
- Ni cha bure kabisa!
- Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!
- Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.
- Ni kijarida chako!
- Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!

Ndani ya Toleo Hili

Walivyoitafuna ATCL	1
Hoja ya Mwanakijiji	1
Walivyoitafuna ATCL	2,3
Ujumbe wa Rev. Kishoka	3
Makala mbalimbali	4
Cheche Pekee na Habari	5
Picha, Katuni na Maoni	6

HOJA YA MWANAKIJIJI — TUTAWALINDA MPAKA LINI?

Kinachoendelea kwenye shirika letu la ndege kinaweza kuelezewa kwa neno moja tu—Aibu!

Jitihada za "kufufua" shirika hilo zimegonga mwamba na bila ya shaka zimefikia kikomo kwani kinachofanyika siyo tena kulifufua bali kuhakikisha kuwa huko lilikofia hata ikilia parapanda ya mwisho haliwezi kuhuishwa tena!

Uongozi wa ATCL chini ya Bw. David Mattaka na Mwenyekiti wa bodi ya shirika hilo Balozi Mustafa Nyang'anyi umedhihirisha kile ambacho rafiki yangu mmoja amezoea kukisema kuwa "Waafrika ndivyo tulivyo".

Inasikitisha kuwa serikali imevumilia ubinafsi, uzembe, na uongozi butu wa Watanzania wenzetu hawa hadi kufikia kutaka kuwaalika Wachina kutuendeshea shirika hili.

Ni aibu kuwa Tanzania haina watu wenye uwezo wa kuendesha shirika la ndege kwa mafanikio. Ama tunao?

WALIVYOITAFUNA ATCL

alishauriwa na wataalamu wake kuwa ATCL haina uwezo wa kufanya safari hiyo lakini kwa shinikizo la Mwenyekiti wa Bodi Bw. Nyang'anyi wakaamua kuuchukua mradi huo na matokeo yake yanakumbukwa kwani ilisababisha serikali kuingilia kati na kuwasafirisha mahujaji wale na kuapa kuwa jambo hilo halitatokea tena.

Tulitarajia (kama watanzania wengine) kuwa kuwa jambo lile lingekuwa somo kwa serikali kuangalia kwa ukaribu utendaji na uongozi wa kampuni hiyo na kufanya mabadiliko ya haraka. Cha kushangaza Balozi Nyang'anyi aliendelea na wadhifa wake na Mattaka aliendelea na wadhifa wake kana kwamba jambo lile lilikuwa dogo tu.

Ukodishaji wa Airbus 320 na Dash8 mbili

Wakati sakata la Mahujaji linatokea uongozi wa ATCL walikuwa mbioni kukamilisha ukodishaji wa ndege aina ya Airbus kutoka kampuni ya Wallis Trading ya Liberia (kampuni yake mama iko Ufaransa). Kabla ya hapo ndege hiyo kubwa ilikuwa ikifanya kazi chini ya shirika la ndege la Air Jamaica lakini baada ya kuacha kutumiwa ilipelekwa El Salvador ambako ndiko ATCL iliifuata.

Ndege hii ilikodishwa kwa mkataba zaidi ya dola milioni 30 kwa miaka mitano, ikiwa na makadirio ya kutengeneza hela nyingi kila mwezi. Wakati kina Nyang'anyi na Mattaka wanasimamia mpango huu ATCL haikuwa imejiandaa kibiashara wala kimkakati wa biashara kuweza kufanya ndege hii iwe kweli ukombozi kwa shirika hilo. Hakukuwa na rubani/marubani wa kitanzania waliokuwa na uwezo wa kurusha ndege hiyo kubwa na ya kisasa; hawakuzingatia ukweli wa biashara ya anga na hasa ushindani uliopo eneo letu hili.

Ndege yenyewe iliponunuliwa ilikutwa na matatizo ndani ya ubovu wa vitu mbalimbali na hivyo kuongeza gharama ya matengenezo kuliko ilivyotarajiwa mwanzoni. Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali kulikuwa na mapungufu zaidi ya 100 ndani ya ndege hiyo ambayo yalihitaji kufanyiwa matengenezo. Kinyume na ilivyosemwa kuwa walichofanya ni kubadili rangi tu (kuweka za Air Tanzania) ukweli ni kuwa ndege ilikuwa na viti vibovu, milango mibovu n.k vitu ambavyo vingine ilibidi wanunue wa "kufunika tu" ili kuficha ubovu (ma-cover ya viti vya abiria).

Wakati huo huo shirika hilo hilo lilikuwa limeingia mkataba wa kukodisha ndege nyingine mbili za Dash8 ambazo nazo zinapendeza kweli kwa nje lakini kutokana na mkakati mbaya wa biashara na kukosekana kwa motisha kwa wafanyakazi (kama tutakavyoona hapa chini) kumechangia kufanya uwekezaji huo kuwa wa hasara kubwa.

Lakini kwenye Airbus kilichoshtua zaidi ni mkataba wa kulipa dola 360,000 kwa mwezi kitu ambacho kilioneshwa awali kuwa wangeweza kupata mkataba mzuri lakini kutokana na ung'ang'anizi wa hawa wawili shirika lakaingia mkataba huu wa kulipa karibu shilingi milioni 370 kwa mwezi karibu shilingi milioni 14 kwa siku! (ndege iwe inaruka au hairuki! Inatengeneza faida au hasara).

Tuliweka mkataba huo hadharani (unaweza kuuona kwenye mwanakijiji.com) na kuhoji kuwa huo nao ni mkataba mwingine wa kifisadi. Wakati ndege inasubiriwa (ilichelewa sana kuja kwa karibu miezi sita) watumishi wa ATCL waliokuwa wanafuatilia ndege hiyo huko El Salvador walikuwa wanalipwa dola 400 kwa siku! Mmoja wao alikaa karibu miezi sita huko. Mmoja wao kwa muda wote huo ameweza kukusanya zaidi ya Shs. Milioni 86!

Viongozi hawa hawa walipofanikiwa kuileta Airbus kwa mbwembwe na kualika waandishi wa habari walijikuta ndege bado inahitaji matengenezo ya hapa na pale na kulazimu kuingia mkataba na kampuni ya Mauritius na inakadiriwa walikuwa wanalipa dola lakini mbili kwa mwezi (jumlisha hizo na zile za Wallis Trading)!

Marubani wa Airbus

Kama ambavyo Cheche imedokeza hapo juu, ATCL haikuwa na marubani waliofuzu kurusha dege hilo kubwa. Kwa muda wote huo (hadi leo hii) kampuni hiyo imekuwa ikitumia marubani wa kigeni (kutoka Uingereza na wengine kutoka Ufaransa). Baadhi yao ni marubani waliokubuhu na wengine inasadikiwa ni marubani wanafunzi! Marubani hao hulipwa karibu Euro 16,000 kwa mwezi (wale First Officers) na wamekuwa nchini sasa kwa karibu miezi sita. Licha ya malipo hayo ATCL inawalipia hoteli wanakokaa na kuwapa posho ya kujikimu wakati wowote ndege hairuki!

Baadhi ya marubani wanaoletwa na kampuni ya EASYWAY inadaiwa kuwa ni wanafunzi na wanakuja kufanya mafunzo yao kwenye ndege yetu ya Airbus 320. Ni uchunguzi huru tu unaweza kuonesha ukweli wa jambo hilo.

Hadi hapo tulipofikia tumeonesha kuwa ATCL inatumia zaidi ya Shilingi milioni 500 kwa mwezi kulipia madeni na majukumu yake! Cheche inajiuliza kwa mtindo huu na kwa mwendo huu shirika hili litaweza vipi kuanza kutengeneza faida?

Marubani hao wanalipwa hotelini karibu dola 150 kwa siku (kwa watu wanne ni dola 600) na kuna kila dalili ya makubaliano ya aina fulani ambapo kuna watu wanapata "kamisheni" ya aina fulani kutokana na malipo hayo makubwa.

Matumizi ya fedha za ATCL

Mojawapo ya vitu ambavyo vimetushangaza sana katika uchunguzi wetu wa kina ni jinsi gani wakuu wa shirika hilo wamefanya ATCL kuwa ni kisima cha utajiri kama wale wa Benki Kuu walivyofanya hivyo au wale kwenye wizara na taasisi nyingine za umma wanapofanya maeneo ya kuwa ni "EPA" yaani mahali pa kujichotea fedha nyingi pasipo kuogopa matokeo yake.

Hadi hivi sasa viongozi wa shirika hilo wanaolia mara kwa mara kwenye vyombo vya habari kuwa shirika halina pesa ndio wamekuwa wa kwanza kukopeshana na kuchota fedha za umma kama za sadaka. Wapo wanaodaiwa karibu milioni 25 katika mikopo yao mbalimbali. Magari yaliyoletwa kwa gharama kubwa mengine bado yako kwenye eneo la kuegeshea huku hajulikani nani atakayeyatoa hapo (baada ya sisi kuliweka jambo hili hadharani miezi kadhaa iliyopita).

Kwa mwaka huu uliopita tu kuna wakurugenzi wa kampuni hiyo katika "safari" zao mbalimbali wameshatumia zaidi ya Shilingi milioni 172. Wizi (tunauita kwa jina lake halali) unaofanywa ni ule wa kutumia kile kinachoitwa "acting allowances" ambapo kiongozi akiondoka makao makuu na na nje ya mkoa au hata nchi basi mtu mwingine anakaimu nafasi hiyo na huyo anayekaimu ukifika mwisho wa mwezi analipwa mshahara wake wa kawaida na posho ya kukaimu!

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

WALIVYOITAFUNA ATCL

Kwa kufanya hivyo wajanja wa ATCL wakiongozwa na David Mattaka wamekuwa "wakikaimiana" kama mazoezi, leo huyu anarudi mwingine anaondoka, na yule akirudi mwingine anaondoka na fulani anakaimu. Vyanzo vya ndani vinadokeza kuwa kiasi cha karibu ya Shs. Milioni 15 zinatumika kila mwezi kuwalipa wakurugenzi posho mbalimbali za kukaimu!

Wizi wa namna hiyo haujaishia kwenye wakurugenzi tu lakini pia ndani ya bodi kwani bodi yenyewe kila wanapokutana wanalipwa na fedha za Shirika. Yawezekana hilo ni jambo la kawaida lakini kwenye taasisi yenye matatizo kama ATCL kuna uwezekano vikao mbalimbali vinafanywa ambavyo ni vya "dharura" na katika vikao hivyo malipo pia hufanyika. Kikao kilichofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita wajumbe wa bodi hiyo walijikuta wakigawana karibu dola 5500 kwa kikao chao cha masaa mawili!

Wakati huo huo hawa wanagawana pesa na kufuja mali ya umma kuna watumishi wengi wa ATCL ambao hawajalipwa mishahara yao au mafao yao mbalimbali. Ni hawa ndio wanahenyeka kila siku lakini sasa wamekata tamaa kama walivyofanya katika tamko lao la mwisho wa wiki kumtaka Nyang'anyi na Mattaka wang'olewe.

Tuliweza kuonesha mapema mwaka huu jinsi wakurugenzi wa shirika hilo walivyoweza kununua magari kutoka Uarabuni huko kwa gharama ya karibu dola laki tatu. Magari hayo baadaye walikuja kujikopesha wakurugenzi wenyewe na Inatuhumiwa watumishi wa ngazi za chini waliohusika na kwenda kuyakagua magari haya uko Uarabuni au kuweka sahihi zao wameongezewa mshahara wao angalau mara mbili!

Ajira za kushangaza
Hivi unavyosoma kijarida chetu hiki tunaweza kusema kwa uhakika mkubwa kuwa kuna manung'uniko mengi ndani ya shirika hili. Kwenye toleo lililopita tuliripoti wizi wa karibu lita 6000 za mafuta ya ndege huko Mwanza. Kuna ajira zinazosumbua watu mbalimbali kwani msingi wake ni kufahamiana na undugu uliokithiri. Kama tulivyoripoti wiki iliyopita hata mradi wa kutengeneza kalenda ya 2009 ambaye anatarajiwa kupewa (kama bado hajapewa) ni ndugu wa Manji (mkuu wa utendaji wa shirika hilo).

Kuna manung'uniko ya ajira zinazotokana na mapenzi ambapo kuna wanaoaminiwa kuwa ni vimada wa watumishi wa ngazi za juu wakipewa nafasi za ajira na mafunzo huku wale waliotumikia ATCL kwa muda mrefu na ambao wanastahili nafasi hizo kwa haki wakirudikwa.

Maneno yamesemwa vizuri na mmoja wa watumishi wa shirika hilo waliozungumza nasi mwishoni mwa juma kutoka jijini Dar "Tatizo la ATCL siyo fedha; tatizo la ATCL ni uongozi na utawala. David Mattaka alipewa nafasi hiyo kwa kujuana na kutoka hapo imekuwa ni ufisadi mbele kwa mbele". Mtumishi mwingine alielezea kuwa "sasa tumechoshwa, hawa jamaa wanahonga hadi waandishi wa habari kama walivyofanya kwenye kikao chao cha juzi".

Swali moja ambalo Cheche inakuachia msomaji, ni je suluhisho la ATCL ni kuwapa Wachina? Je ni kweli katika Tanzania hatuna watu wenye uwezo wa kuendesha shirika hilo kwa faida? Je serikali iamue kuliuza shirika hilo kwa wazawa na kuachana na biashara ya safari za anga? Je kama kina Mramba na Yona wamefikishwa mahakamani kwa kulisababishia Taifa hasara kubwa, je hawa kina Mattaka na Nyang'anyi watafikishwa lini kizimbani kwa makosa ambayo hatuna shaka ni ya kihalifu? Je watumishi wa ATCL nao wagome ili jambo lifanyike?

UJUMBE WA REV. KISHOKA "Mhe. Mwenyekiti…"



Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, maarufu kama AU, Bwana Jakaya Mrisho Kikwete, naomba utege sikio umsikilize Mchungaji.

Najua nimekuwa nikiongelea sana kuhusu mambo ya ndani ya nchi yetu na kukutaka usimame kidete kusafisha uozo ulioleta Ufisadi, Uzemba na Uhujumu. Naam nashukuru kwa taratibu umeeanza kazi.

Lakini safari hii Bwana Muungwana, Mchungaji anaongelea nafasi yako kama Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Kiafrika.

Naomba utumie utashi wako kutatua matatizo ya Afrika bila kumuonea haya mtu!

Ulimtumia Membe kutoa tamko kuhusu Sudan, wakati jirani wa Kenya walipopata msukosuko wakati wa uchaguzi, sauti yako haikusikika. Ukasaidia Serikali ya Comoro iondokane na ugaidi.

Lakini kuna mambo ambayo yanahitaji sauti yako ya ukali na uongozi mahiri ukitumia uzoefu wako katika masuala ya mambo ya nje na kimataifa.

Nakuomba wakati unamalizia muda wako kama Mwenyekiti wa AU, utuletee ufumbuzi Zimbabwe ambako ukatili wa ndugu yetu wa awali wa mapambano, Robert Gabriel Mugabe unatishia si uhai wa Raia wasio na makosa pekee, bali ni hatari kwa usalama wetu kusini mwa Afrika.

Aidha inabidi uwakalishe chini kina Museveni na Kagame na waambie waache kumsaidia Jenerali Nkunda ambaye analeta vurugu Kongo.

Na mwisho, sauti yako inahitajika ma kwa kupeleka Jeshi lakulinda Amani au kuunda kamati ya usuluhishi ili kuleta Amani na kuwepo kwa Serikali katika Jamhuri ya Somalia.



Raila Odinga katoa kauli ambayo inaonyesha ujasiri kwa kutaka Mugabe awajibishwe, swali langu kwako je uko tayari kusimamia haki za binadamu na demokrasia Afrika kwa kumshurtisha Mugabe aachane na ubabe wake

Je uko tayai kuwakalisha chini zile koo pale Mogadishu ambazo sasa zinatambaa Bahari ya Hindi kuteka meli ili Somalia iwe na Serikali?

Je kule Afrika Magharibi anzia Nigeria, Sierra Leone na kwingine utulivu tunaounona ni wa kweli au ni mazugazuga?

Nakuomba basi uchukue hatua kubwa katika uenyekiti wako kuhakikisha unahamasisha uwajibikaji wa viongozi, kuimarika kwa Demokrasia na Kulinda haki za Binadamu ikiwa ni ziada ya cvita ya kutetea maslahi ya kiuchumi ya Afrika.

Ni hayo tuu Ndugu Mwenyekiti.

TUCHUKUE SHERIA MKONONI?

Na **Jessica L Fundi**



Mojawapo ya matukio ya kusikitisha na kushangaza yametokea wiki iliyopita ambapo watoto wawili wa shule ya msingi waliuawa kinyama na kile kinachodaiwa kuwa "kundi la watu wenye hasira".

Watoto hao Emmanuel Malobya (16) na Bakari Ramadhani (14) walikuwa wanafunzi wa shule ya Msingi Manzese jijini Dar-es-Salaam. Kwa mujibu wa vyombo vya habari miili ya watoto ya watoto hao ilifikishwa katika hospitali ya Mwananyamala baada ya watoto hao kuuawa kwa madai ya kuiba vioo vya gari.

Cha kushangaza ni kuwa hakuna mtu aliyejitokeza kudai kuwa gari lake ndilo limehusika au ni yeye aliyeitia watoto hawa wezi. Lakini cha kuudhi ni kuwa watu wazima walioshuhudia jambo hili (kama wapo) walikuwa hawana ubavu wa kuwadhibiti watoto hawa ambao hawakudaiwa kuwa na silaha yeyote na kuwafikisha kwenye kituo cha Polisi au kwenye uongozi wa mtaa.

Tunapofikia tunaua watoto wadogo namna hii kwa sababu ya mtu kaita "mwizi" basi tunathibitisha kuwa bado tunaishi na fikra za kijima ambazo zinaongozwa na hulka (instincts) za kinyama.

Inakuwaje basi leo tunajifanya tunashangaa mauaji ya Albino wakati kwa miaka nenda rudi kumekuwa na mauaji ya vikongwe na wanawake wazee kwa tuhuma za uchawi?

Inakuwaje leo tunashtushwa na mauaji ya Albino wakati miaka nenda rudi watu wamekuwa wakichomekwa matairi ya magari na kumwagiwa petroli kwa kudaiwa ni "kibaka"?

Baadhi ya watu wanaoshiriki katika mauaji haya wao wenyewe hata hawajui kosa lenyewe au hata kumjua anayedai kutendewa kosa hilo. Watu wanachukua mawe, fimbo na wengine kurusha ngumi na mateke kwa sababu fulani tu kaoneshewa kidole cha wizi.

Wazazi wa watoto hawa wamedai pasipo shaka kuwa watoto hawa hawakuwa na tabia hiyo na hakuna mtu hata mmoja aliyejitokeza kusema amewahi kutendewa kitendo cha kihalifu na watoto hawa.

Hatutashangaa kwa serikali kukaa kimya na kufanya uchunguzi kama ule wa Tabora ambapo Polisi wanausimamia. Kama vile Tabora watuhumiwa ni wale wanaochunguza!

Kwa mujibu wa gazeti moja lililotolewa wiki iliyopita mmoja wa wazazi wa watoto hao "anaamini kuwa mtoto wake aliuawa na askari waliokuwa lindoni katika hoteli moja iliyopo katika eneo hilo la Legho."

Wakati umefika kwa Watanzania kuanza kukataa tabia hizi za kinyama na ambazo zimejaa unafiki wa wazi. Tunapofikia kuanza kuua watoto wadogo namna hii na kujichukulia sheria mikononi inaonesha ni jinsi gani bado tunasafari ndefu ya kustaarabika na kuelimika kwani baadhi ya watu wanaofanya vitendo hivi yawezekana kabisa ni watu ambao jamii inawaona ni "wasomi" au "waliolimika".

Tusipofanya hivyo, tutaanza kuishi kama kwenye shamba la wanyama!

HOJA YA NGUVU

MAHAKAMA YA WAHUJUMU UCHUMI IUNDWE!

Na. **Benjamin Mwalukasa**

Makosa ya Kuhujumu Uchumi kwa mujibu wa sheria ya Uhujumu Uchumi ya mwaka 1984 yatasikilizwa kwenye Mahakama ya Makosa ya Kiuchumi (Economic crimes court).

Mahakama hii kwa mujibu wa sheria inaundwa na Jaji wa Mahakama Kuu na kwa mujibu wa sheria inakuwepo pale ambapo Mahakama Kuu inasikiliza makosa ya Kuhujumu Uchumi na hivyo kufanya Mahakama hiyo kuwa ni ya Makosa ya Kiuchumi.

Ninafahamu kuwa DPP anaweza kuamua kupeleka kesi za makosa ya kiuchumi kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi, hata hivyo ninaamini kuwa kufungua kesi za makosa ya kiuchumi kwa mujibu wa sheria hiyo na kuacha Mahakama ya Makosa ya Kiuchumi kufanya kazi ndilo jambo bora zaidi na lenye mantiki.

Kwanza, ni kwa sababu makosa ambayo yanadaiwa kutendwa wakati huu ni makosa ambayo kwa kila kipimo ni makosa ya kiuchumi.

Unapoleta watu mahakamani kwa makosa ya wizi mkubwa wa Benki Kuu, mahakama sahihi ni Mahakama iliyoundwa kushughulikia makosa hayo.

Pili, jinsi makosa haya yalivyoletwa kwenye mahakama ya Hakimu Mkazi (Kisutu) na kugawanywa kwa mahakimu mbalimbali wakati tuhuma zinahusiana na mtiririko wa matukio unahusiana ni wazi kuwa tuhuma hizi zinahitaji kushughulikiwa kwa pamoja.

Tatu, kutokana na hilo la pili hapo juu, kuunda Mahakama ya Makosa ya Kiuchumi kutamuweka Jaji wa Mahakama Kuu kusimamia kesi hizi na hivyo kuondoa mlundikano wa kesi katika Mahakama ya Kisutu.

Nne, kwa vile sheria inasema kuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu anayepaswa kusimamia mahakama ya aina hii, ni wazi kuwa jambo jepesi na linalowezekana ni kwa Rais Kikwete kuteua majaji angalau watatu au wanne wapya wa Mahakama Kuu (wanaweza kuwa walio Mahakamu Wakazi wanaosikiliza kesi hizo sasa) na kuwapa jukumu moja tu nalo ni kusikiliza kesi za kiuchumi zote ambazo zimeanza kushughulikiwa sasa.

Mashtaka ninayoyazungumzia siyo haya y a kina Mramba na Yona bali haya ya kina Jeetu Patel na wenzake na wale wote wanaodaiwa kushiriki katika wizi wa fedha za Benki Kuu toka akaunti ya EPA.

Wizi huu ni mkubwa mno na ninaamini tukianzisha mahakama hiyo maalum ambayo inawezekana kisheria, tutaweza kuanza kushughulikia makosa haya bila kuingilia mchakato wa mahakama za kawaida.
Tuifanye mahakama hiyo ya kudumu.

Soma Bure
hoja zenye nguvu

CHECHE PEKEE

DOWANS KUPEWA MSHIKO?

Na. Mahmoud Rashid

Kuna mchezo unapangwa kuchezwa mchezo ambao wachezaji wake ni wale wale isipokuwa walichobadilisha ni jezi tu.

Tatizo la mchezo huu ni kuwa licha ya kuwa wachezaji ni wale wale, marefarii no ni walewale, uwanja ni ule ule na hata washangiliaji wale wale.

Kampuni ya Dowans ambayo tuliambiwa imerithi mkataba wa Richmond bado inashikilia majenereta yake baada ya serikali kuvunja mkataba nayo.

Tatizo ni kuwa kampuni ya Dowans haikurithi mkataba halali kwani kampuni ya Richmond haikuwa na mkataba halali na TANESCO!

Sasa kama hakukuwa na mkataba halali kati ya Richmond na Dowans (kwa vile Richmond haikuwa kampuni halali hapa Tanzania) inakuwaje basi kuingia mkataba na kampuni nyingine ambayo nayo inamaswali yale yale ya kwenye mkataba ambao tumeuvunja?

Tayari tulikuwa tunailipa Dowans shilingi karibu milioni 160 kwa siku wakati tunajua/tulipaswa kujua mkataba wao haukuwa halali, na sasa hakuna mtu yeyote aneyezungumzia kurudishiwa fedha zetu (japo kiasi) na wataalamu wetu wanataka bado kuwapa ulaji watu wale wale.

Tatizo jingine ni kuwa hatujui hasa Dowans ni kampuni ya kina nani hasa. Wakati wamechukua mkataba na Richmond tuliambiwa kuwa Dowans ni kampuni kutoka Uarabuni (yawezekana kuwa kweli kuna jina la Afisa mmoja wa Kijeshi toka nchi mojawapo ya kiarabu ambaye jina lake linahusishwa na Dowans).

Baadaye tukaambiwa kwenye vyombo vyetu vya habari kuwa Dowans ni kampuni ya Afrika ya Kusini ingawa huko Afrika Kusini hatujui iko kwa jina gani na maafisa wake ni kina nani (kuna mahusiano ya ajabu ya baadhi ya makampuni ya kifisadi na Afrika Kusini). Lakini tena katikati ya mwaka huu tukaambiwa (na Dr. Rashid wa Tanesco) kuwa kampuni hiyo makao yake makuu yako Costa Rica! (Angalia Gazeti la Tanzania Daima la Julai 1)

Kingine cha kushtua ni kuwa kwa mujibu wa Kamati Teule ya Bunge katika ripoti yake iliyosomwa na Dr. Mwakyembe ilionesha kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Usambazaji wa Tanesco Bw. Mohammed Saleh alikuwa ni rafiki wa wamiliki wa Richmond na baada ya kustaafu tu "akawa mmoja wa Wahandisi waandamizi wa Dowans SA".

Vyanzo vyetu hata hivyo vinadokeza kuwa waliohusika na Richmond hawajakubali kushindwa bado na wanajua bei ya majenereta yao ilikuwa ya kurusha mno na hata wakiuza kwa nusu yake bado watapata faida.

Hata hivyo baadhi ya wabunge wa CCM ambao wanafahamu suala hili kwa undani wameapa kuwa "hakuna cha Richmond wala Dowans majenereta yao hatununui". Kwa mujibu wa Mbunge mmoja ambaye ni mkimya sana "hawa hawawezi kutuingiza tena mjini kama tunataka majenereta tutanunua kwa watengenezaji sisi wenyewe hatuhitaji hii mitumba yao".

Mbunge wa Ukerewe Mhe. Getrude Mongella alitoa pendekezo lifuatalo kwenye kikao kimoja cha Bunge "Serikali isiishie hapo kwenye kusitisha mkataba tu, ingeenda mbele zaidi ikataifisha mitambo ya Dowans, ili iisaidie nchi katika kipindi utakapohitajika umeme wa dharura"

Vinginevyo Dowans tukiwalipa tena Ngeleja ajiandae kung'olewa!

GRAY MGONJA AFIKISHWA KIZIMBANI

Na Mwandishi Wetu

Aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Bw. Gray Mgonja amefikishwa mahakamani kwa mashtaka nane ya kulisababishia taifa hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 11 na mia saba kutokana na uzembe na matumizi mabaya ya madaraka akiwa ni mtumishi wa umma.

Kwa mujibu wa mwendesha mashtaka wa serikali Bw. Fredrick Manyanda Bw. Mgonja alifanya hivyo katika kutoa msamaha wa kodi kwa kampuni ya Alex Stewart kati ya mwaka 2003 – 2007. Bw. Mgonja ambaye alisimamishwa mbele ya Hakimu Mkazi Hebron Mwankenja alikana mashtaka yote dhidi yake.

Hakimu Mwankenja alisema kuwa dhamana ya Bw. Mgonja iko wazi na alitakiwa kuleta mahakamani fedha au mali inayolingana na thamani ya Shs bilioni 5.9. Bw. Mgonja alishindwa kutimizia sharti hilo. Pamoja na hilo mahakama ilimuamuru Bw. Mgonja kusalimisha hati yake ya kusafiria, pamoja na kutoondoka Dar bila idhini ya mahakama.

Kesi ya Bw. Mgonja inatarajiwa kuunganishwa na ile kesi no 1200 inayowakabili Mawaziri wa Zamani Basil Mramba na Daniel Yona ambao wote wanakabiliwa na mashtaka ya uzembe na kulisababishia Taifa hasara kuhusiana na msamaha huo wa kodi wa Alex Stewart.

Licha ya tuhuma hizo za kodi Bw. Mgonja bado anatajwa katika kashfa nyingine kadha wa kadha ambazo zinamhusisha yeye kama Katibu Mkuu na mtu binafsi.

Kubwa zaidi ni pale ambapo jina lake lilionekana katika kampuni TANGOLD ambayo iliandikishwa nje ya nchi. Kampuni hiyo ilipoandikishwa Tanzania wanahisa wake walikuwa ni yeye Mgonja, Gavana Ballali na Mhe. Andrew Chenge (a.k.a V. G. Cent). Wengine ni pamoja na Patrick Rutabanzibwa (Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Vincenti Mrisho (alikuwa Katibu Mkuu Ulinzi) aliyestaafu pamoja na Mgonja siku chache zilizopita.


Tatizo ni kuwa kampuni ya Tangold haioneshwi mahali popote katika mahesabu ya serikali kuwa ni ni mali ya serikali aidha kwa ujumla au kwa sehemu.

Cheche inaendelea kufuatilia kesi hizi na tunatarajia washukiwa wengine wa ufisadi ambao wanahusiana na Mgonga katika kesi hii wako njiani kufikishwa kizimbani.

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...


KATUNI ZA WIKI

Picha za Wiki



Bw. Gray Mgonja alipofikishwa mahakama ya Kisutu jana Chini wacheza wa Taifa Stars wakia na Waziri Seif Khatib





PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia sisi!

KUTOKA KWENYE MTANDAO

Bado siamini kama kweli hizi kesi za mafisadi zitazaa matunda yoyote ya maana ingawa vile vile sina sababu ya maana ya kutoiamini serikali hii kuwa inafanya ukweli—**Kichuguu**

Na ni kwanini ofisi ya DPP ndio inashitaki na sio TAKUKURU? Huyu DPP analeta kesi zinazo onekana kama vile "administrative misjudgement" zilizosababisha hasara. Hawawashitaki kwamba wamejineemesha na rushwa. Kama hakuna ruswha kwanini kuwahusisha TAKUKURU basi? **Kuhani**

Hii habari ni ya kuhuzunisha sana, ndio jamii yetu hii tunayoishi, poor boys na i bet hii tukio litapita hivi hivi kama la wale watoto waliokufa Tabora, hicho ndicho kinachonisikitisha zaidi.—**Megz**

Hao wakina Masha,Makamba,Hosea, Mchikali na viongozi wengi katika serikali yetu na taasisi mbalimbali za Umma kwa kauli zao zisizo na kichwa wala miguu zimekua kichefuchefu kwa wengi kwa sababu hawajui nini wanachokisema na wapi wanapotoa kauli zao—**Advocate Jasha**

Kama DPP anataka kufanya kweli na watu waamini kuwa huyo bwana Feleshi ofisi yake kweli iko huru basi ampandishe kizimbani advocate Malegesi!! Ama sivyo mnatupiga madongo ya macho tu sisi wadanganyika!! - **Bulesi**

Tunarudia tena kutamka waziwazi kwamba CCM haina uhusiano wa aina yoyote na Kagoda na hivyo shutuma zinazotolewa na Zitto na wapinzani wengine ni za uzandiki mtupu, ni siasa zenye takataka zinazolenga kukipaka matope na kukijengea chuki kwa wananchi... Hivyo vijana wadogo waliolelewa na CCM wanapoanza kukipaka matope wanatafuta laana na njama zao hazitafanikiwa!

"Wamezaliwa wameikuta CCM ni imara na watakufa wataiacha imara, CCM sio mtu, ni umoja wa mamilioni ya Watanzania wenye nia safi na ndiyo maana CCM inaaminiwa na kuheshimika ndani na nje ya nchi—**John Chiligati**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mwanakijiji@mwanakijiji.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*